**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OWM-TAMISEMI)**

**SHULE YA SEKONDARI MPUI,**
**S.L.P 338,**
**SUMBAWANGA.**
**02/05/2026.**

**Namba za Simu: -**

**Mkuu wa Shule: 0766480580/0621050499**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0764428425**

**Matron: 0757571243**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………..........................................................................**
**S.L.P…………………………………... …………………………………………….......**

YAH**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MPUI K**

**1.** Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika **SHULE YA SEKONDARI MPUI** mwaka **2026** kwa tahasusi ya **HGL/HGLi.**

Shule ya Sekondari MPUI ipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa ina umbali wa Kilometa 55 kutoka Sumbawanga mjini ipo Mashariki mwa Mji wa Sumbawanga. Usafiri wa basi kutoka Sumbawanga mjini unapatikana katika kituo cha mabasi **Katumba** na nauli kati ya Shilingi 4,000/= hadi 5,000/= kwa usafiri wa hiace zinazoelekea mji wa Laela. Aidha kwa wale wanaotokea barabara ya Mbeya - Sumbawanga unapaswa kushukia kituo cha **Mpui ya UFIPA** na Shule ipo umbali wa mita 20 upande wa kushoto, Kutoka kituo cha kushukia.

**2. MIHULA YA MASOMO;**

Kwa kidato cha **TANO mihula ya masomo** inaanza mwezi wa saba (Julai) ambapo Shule itafunguliwa tarehe **…………..** Hivyo mwanafunzi anapaswa kuripoti Shuleni tarehe **……………** na mwisho wa kuripoti kwa kidato cha **TANO** ni tarehe **…………..** Muda wa kuripoti ni kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni na kwa anayetokea mbali toa taarifa mapema ili kupata msaada zaidi.

**3. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**(a) Sare za Shule**

I. Sare ya Shule ni sketi mbili za draft (kitambaa kizito). Sketi iwe ndefu inayofika chini na kugusa viatu mfano wa kitambaa umeambatishwa na mshono rinda box uwe makini kutokuchanganya rangi pia mfano wa kitambaa unapatikana Shuleni.

II. Shati la Shule ni rangi ya blue bahari (**TETRON**) yenye mikono mirefu ili kuepuka kuchanganya sare mfano unapatikana Shuleni.

III. Tai mbili rangi za sketi.

IV. Rangi ya hijabu (kijuba) iwe blue bahari (**TETRON**)ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

V. Sare ya Michezo kwa Shule hii ni track suti rangi ya bluu bahari na raba nyeupe za michezo jozi moja na **sare hii ya michezo ivaliwe na mwanafunzi siku ya kuripoti Shuleni.**

VI. Viatu vya Shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye **visigino vifupi** na viatu vyenye visigino virefu (high heels) haviruhusiwi.

VII. Soksi jozi mbili rangi ya **blue** ndefu (stockings), na siyo w

VIII. Sweta moja la rangi ya DARKBLUE na kaba shingo rangi nyeusi kwa ajili ya kujikinga na baridi kipindi cha baridi.

IX. Nguo za kushindia (*shamba dress*) ni magauni mawili mshono wa solo iwe ndefu ifike kwenye fundo la miguu, mfano wa kitambaa upo mwisho wa fomu hii na pia mfano utapatikana Shuleni ili usichanganye rangi.

X. T-shirt ya kushindia rangi ya gold yenye kola.

**MUHIMU**

- ❖ **Mwanafunzi aje na Bima ya Afya siku ya kuripoti kwa ajili ya matibabu yake.**

- ❖ **Mwanafunzi aje shuleni na nakala halisi ya matokeo ya kidato cha nne (Form IV Result slip original) kwa ajili ya uhakiki.**
- ❖ **Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani nje ya maelekezo hapo juu na siku ya kuripoti avae track suit kama ilivyoelezwa hapo juu.**

(b) **Mahitaji mengine muhimu**

i. Madaftari counter books 7 (3 quire)
ii. **Ream(A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka.
iii. Godoro moja la futi 2.5
iv. Mashuka Jozi 2 rangi ya pinki, blanket 1, foronya ya godoro1, chandarua1.
v. Nguo za ndani za kutosha;
vi. Vyombo vya chakula (sahani,bakuli,kijiko na kikombe viwe vya bati).
vii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

**Vifaa vya usafi**

**I. Kwanja 1,**
**II. Jembe 1 lenye mpini,**
**III. Reki 1,**
**IV. Fagio 1 za chelewa,**
**V. Soft/hard broom 1**
VI. **Squizer** 1.

**(c) Michango mbalimbali**

**A. KWA KIDATO CHA TANO MICHANGO ITAKUWA KAMA IFUATAVYO;**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi (Tsh.)** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

**NB: Michango hii ilipwe kwenye Akaunti NAMBA. 62102300244 – NMB, yenye jina MPUI SECONDARY SCHOOL.**
**Siku ya kuripoti mwanafunzi aje na Karatasi ya Benki au Wakala ya malipo (Pay in Slip).**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizaraya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu –TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada yakuripoti Shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule.

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima. Wanafunzi wanatakiwa kusimama na kumsalimu mwalimu/mtu yeyote anayewazidi umri anapopita,anapoingia darasani au kwenye kumbi za mikutano.
ii. Kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa Serikali,nembo ya Taifa (Coat of Arms) na wimbo wa Taifa.
iii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya shule;
iv. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
v. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
vi. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vii. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
viii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
ix. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
x. Kutunza mali za shule;
xi. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xii. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

- **MIPAKA YA SHULE.**

  (i) Wanafunzi hawaruhusiwi kutoka nje ya Shule isipokuwa kwa kibali maalum.

  (ii) Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum
  a) Ofisi za walimu (Staff room).
  b) Ofisi zingine za Shule.
  c) Maabara (laboratories).
  d) Jikoni (Kitchen)
  e) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana na mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo Shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa Shule;
vii. Kufuga kucha ndefu.
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa na Picha za Viongozi wa Kitaifa.
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu.
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3.3 Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na Shule; na
iv. Picha mbili (2) passport size za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi Shuleni pamoja na namba zao za Simu.
v. Picha mbili (2) passport size za mwanafunzi kwa ajili ya jalada lake.

**4.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwa fahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NIVEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZILIZO AINISHWA HAPO JUU.**

**Mwanao anakaribishwa Shuleni, asome kwa bidii ili apate taaluma stahiki. Aidha tunaomba ushirikiano wako pindi mtoto wako awapo Shuleni.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MPUI.**

**............................**

**JANETH M. AKO**

**MKUU WA SHULE**.

**VIAMBATA VYA RANGI YA SARE ZA SHULE.**

1. **Kitambaa cha Sketi ya kwanza rangi ni draft ya dark blue na Siyo nyeusi.**



2. **Kitambaa cha sketi ya pili.**



3. **Kitambaa cha Shamba dress (Nguo ya kushindia).**



**AHADI YA KUTII NA KUFUATA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE.**

Kama unakubaliana na masharti haya ya kujiunga na shule hii, tunaomba **mzazi** au **mlezi** wa mwanafunzi usaini ukurasa huu na urudishe shuleni, ili kuondoa usumbufu.

**AHADI YA KUTII NA KUFUATA SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE.**

**Mimi Mzazi/Mlezi /Mwanafunzi,** kwa makini nimesoma na kuelewa vema sheria na kanuni za shule, niko tayari kuzifuata kama zilivyo.

**Jina la mwanafunzi** ________________________________________________

**Sahihi**____________________________**Tarehe**__________________________

**Jina La Mzazi/Mlezi**_________________________________________________

**Namba ya Simu**__________________________/_________________________

**Sahihi** ____________________________ **Tarehe** ________________________

**(1) MWISHO**

Mwanao anakaribishwa shuleni, asome kwa bidii na tujitahidi kumpa taaluma stahiki. Aidha tunaomba ushirikiano wako pindi mtoto wako awapo shuleni.

MPUI SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX. 338,
SUMBAWANGA.
02/05/2026.

Medical Officer,
Government hospital,
P.O.BOX……………
………………………

Dear Sir/Madam;

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

STUDENT'S FULL NAME: ___________________SEX: _______AGE: ____________

1. Blood Examination: Haemoglobin (_________________) any observation

---------------------------------------------------------------------------------------------

2. Stool examinations _______________________________________________
3. Urinalysis _______________________________________________________
4. T.B. Tests ________________________________________________________
5. Eyes ___________________________________________________________
6. Chest ___________________________________________________________
7. Ears ___________________________________________________________
8. Abdomen ________________________________________________________
9. Other Observation _______________________________________

EXAMINER'S COMMENT: ____________________________________________

NAME OF EXAMINER ____________________________________ DESIGNATION
________________

SIGNATURE: __________STATION ______________ DATE ______________

OFFICIAL STAMP.

(**Fomu hii irudishwe Shuleni ikiwa imejazwa kikamilifu.)**